

CONSTITUTION OF KENYA REVIEW COMMISSION

(CKRC)

VERBATIM REPORT OF

CONSTITUENCY PUBLIC HEARINGS,

BUTERE CONSTITUENCY,

AT LUNZA SEC. SCHOOL

ON

02/08/02

CONSTITUENCY PUBLIC HEARINGS, BUTERE CONSTITUENCY AT LUNZA SEC, SCHOOL ON 02/08/02

Present:

Com. Salome Muigai

Com. Dr. Mohamed Swazuri

Secretariat Staff in Attendance:

John Watibini - Programme Officer

Gladys Gichuki - Asst. Programme Officer

Asha Boru - Verbatim Recorder

The meeting was called to order at 9.45 by Com. Salome Muigai as the chairperson.

Com. Salome Muigai: Rasmi na kikao cha dharura cha Tume, lakini kabla hatujaanza ningetaka kumwomba mmoja wenu atufungulie kwa maombi tafadhali.

Mwenyezi Mungu Baba, haishie milele, tunasema ni asante kwako Baba, tunatoa Tume hii kwa mkona wako, katika tarafa hii yetu ya Butere, na Baba twakabishi mkononi mwako, kila mmoja ambaye amekuja kwa ajili ya kutoa maoni yake baba, wewe mwenyewe upate kuwalinda na kuwasaidia, watakapokuwa wakiwasilisha maoni yao Baba, nguvu ya roho mtakatifu ipate kuonekana kwako. Asante Baba Mtakatifu kwa ajili ya siku hii, tumeiombea na tumeitazamia kwa muda mrefu. Ingawa Baba katika kikao hiki, tunamkumbuka commissioner ambaye ameaga, Baba Oki, ukae pamoja naye. Linda roho yake, na sasa

wenzake ambao anafanya nao kazi Baba, watakapo maliza kazi hii kwa wakati unaofaa tutasema ni asante. Mkono wako Baba upate kutukumbatia, tunapoanza na tutakapomaliza, kwa Yesu Kristo aliye Bwana. Amen.

Asante sana kwa maombi. Sasa ningetaka kuwajulisha sisi ni akina nani. Nina mwenzangu, mwanakili mwenzangu mwenye atawambia Jina lake, hili msikie pia sauti yake.

Com. Swazuri: Hamjambo, mimi naitwa Mohammed Swazuri, ni Mwanatume.

Com. Salome Muigai: Nami jina langu ni Salome Wairimu Muigai, na mimi ndio nitakuwa Mwenyekiti wa kikao hiki. Pia tumeandamana nasi, wafanyikazi kutoka ofisi yetu, tuna mfanyikazi aliye mkubwa wa wale wengine hapa, kwenye Kikao hiki.

John Watibini: Mimi naitwa John Watibini, hamjambo.

Com. Salome Muigai: Na pia na mwenzake mwenye kumsaidia kunakiri maneno.

Gladys Gichuki: Mimi naitwa Gladys Gichuki, habari zenu.

Com. Salome Muigai: Na pia tuna mwingine pale, mwenye kunasa sauti zenu moja kwa moja.

Asha Boru: Hamjambo, naitwa Asha Boru.

Com. Salome Muigai: Na pamoja nasi, pia leo tuna coordinator wetu wa kutoka hii district, tutamwomba asimame, na pia hawajulishe wana kamati wake wa kutoka constituency ama kikao hiki cha Bunge.

Coordinator: VERNACULAR. Niko na wenzangu ambao tumekuwa tukisaidiana nao kazi, kuhusu Katiba, ndio wamewezesha sisi kuwa hapa leo. Nitawaomba wasimame, na kila mmoja atakuwa anasema neno moja na jambo, thank you.

Imbayi Peter: Mimi ninaitwa Imbayi Peter Morris, ninawakilisha vijana.

Mary Otari: Hamjambo wote, kwa majina ni Mary Otari Wandati, kutoka Marama Central, nawakilisha wanawake.

Judy Kakasa: Hamjamboni, kwa majina naitwa Judy Kakasa, nawakisha N.G.O.

Ruth Otieno: Bushere Vusi, Ruth Otieno, nawakilisha Marama North, na mimi ndio mwandishi wa kamati yetu ya Butere, asante.

Sasa ningetaka kuwaeleza utaratibu tutakaofuata kutoa maoni yetu ya leo. Kwanza kwa lugha, sisi kama wanatume, ama kwenye tume, tunatumia lugha mbili, lugha ya Kiswahili na lugha ya Kingereza, kwa hivyo una uhuru wa kutumia lugha yoyote hiyo. Lakini ikiwa hauwezi, ama huoni, unaweze kujieleza, kwa hivyo lugha pia unaweza kutumia lugha ya mama. Itatubidi kumpata mtu wa kutafsiri. Mara nyingi tukitumia lugha ya mama kama vile tunavyojua, inachukuwa mara mbili ya wakati, kwani mtu mmoja atazungumza na mwingine atafsiri. Kwa hivyo, kama wewe unaweza kujieleza kwa Kiswahili, hata kisio sanifu, sisi wote hatujatoka Mombasa, isipokuwa mwenzaangu Mwalimu Swazuri hapa, wengine, hatuna hiyo lugha kabisa, lakini, kama unaweza tu kujieleza tukakuelewa, basi hiyo Kiswahili kinasosha, ndio tuweze kupata nafasi ya watu wengi kuzungumza.

Pia, tuna utaratibu pia, ya ile unaweza kujieleza. Unawezakuwa wewe unamjadala wako, ama una memorandum yako, unaweza kutupatia tu hiyo memorandum, ukajiandikisha, basi ukaenda shughuli zako, ama ukaketi kusikiliza wenzako. Unaweza kuwa pia una hiyo memorandum yako, lakini ungetaka kuangazia maneno machache juu yake, hatutapeana wakati wa kutosha wa kusoma memorandum neno kwa neno. Kwa sababu mbili, moja ni kuwa, memorandum zingine ni refu kabisa hatutapata nafasi ya kuisoma, kwani kila mtu akija hapa anapata dakika tano peke yake.

Sababu ya pili nikuwa, sisi wanatume, ni kazi yetu kuisoma memorandum yako, neno kwa neno. Sisi tulio hapa, na pia wenye hawako hapa pamoja nasi. Kwa hivyo tafadhali ukitupa memorandum, ujuwe tutaisoma.

Unaweza pia kuwa ujaandika maneno yoyote yenye utatwachia, lakini ungetaka kujieleza tu, kwa maneno yako ya mdomo, ama pengine umejiandikia tu notes zako za kukumbusha vile unataka kusema. Basi nawe pia tutakupa dakika tano, ujieleze. Ukimaliza kuzungumza, tuta, naomba radhi, hizi simu zinatua sana. ukishamaliza kutueleza, wanatume wanaweza kukuuliza maswali, lakini hii maswali yenye tunakuuliza sio ya kujitetea, sio ya kuuliza kwa nini. Ni maswali ya utueleze, utufafanulie hili tukuelewe vilivyo, tukuelewe vile unataka kutuambia. Kwa hivyo tunaweza kukuuliza swali moja, mbili ama matatu, hili ufafanue mambo yako.

Pia ningetaka kusema hili ni jambo halali, ni jambo lenye limeidhimishwa na Bunge, limeidhimishwa na sheria. Kwa hivyo usiogope mtu yeyote kutoa maoni yako. Hii ni jambo lenye limekubaliwa, ni jambo ya taifa, na maneno yenye utazungumza hakuna mtu mwenye atakufuatia, kukuuliza kwa nini uliambia kamati hivi ama vile. Hii ni jambo yenye kila mtu anazungumzia, wana siasa, polisi, kila mtu aliye mkenya, ana nafasi ya kuzungumzia, na uhuru wa kuzungumzia vile vyenye angetaka kusema. Pia watoto, wanaume, wanawake, hata watu wenye ulemavu, kila mtu anakubalia kuchangia maoni yake. Kwa hivyo tafadhali jisikie huko uhuru, kusema yote uliyo nayo. Tumekubaliana dakika ni tano. Usingojee nikuambie zimeisha, zimeisha, zimeisha, nikikuambia mara ya kwanza, tafadhali tumalizie, ndio mtu mwingine apate nafasi.

Sasa ningetaka kumwita mzungumzaji wetu wa mwanzo, na huyo ni Obunaka Shikumo or Shirumo? Shikumo, Obunaka Shikumo karibu.

Jambo moja kabla hajaanza, ukianza unaanza na jina lako, hili iwe kwenye kanda letu, na pia ukishamaliza unaenda kwa Mr. Watibini, kujiandikisha kuwa umezungumza, asante

Obunaka Shikumo: Okay, my names are Obunaka Shikumo, I am representing St.Valarie youth group. St. Valerie youth group, wish to state the following proposals and views, as pertains to the constitution of Kenya, as our motherland, as here below.

Language; language used in the constitution, should be simple, for every Kenyan to be able to understand.

Preamble; the Kenyan constitution, should have a preamble. Should ensure separation of powers, executive, legislature and judiciary.

Legislature;

- a) Age of voting, to remain 18 years, onwards.
- b) Age of parliamentary aspirants, to be 21 years up to 68 years.
- c) Members of Parliament should serve for two terms of five years each, and once, one fails to recapture the seat for the second term, then he or she, should not qualify to make a third attempt.
- d) The people should have a right to recall the M.P, if he fails to deliver, through an opinion vote, where five thousand votes will enable an impeachment of the M.P.
- e) The constitution should cater for independent candidates.

Presidency;

- a) The age to be 35 years up to 68 years.
- b) The president should not be an M.P.
- c) The term of presidency should be limited to two terms, of five years each. And once one fails to recapture the office for the second term, then he or she should not qualify to make a third attempt.

- d) Presidential elections, should be separated from parliamentary elections, and should come first.
- e) The president should only resume office, on securing 65% of the votes registered voters.
- f) The constitution should cater for independent candidates.
- g) The constitution should ensure, level ground for all candidates.

Provincial Administration should be transferred to Public Service Commission.

The post of Assistant Chief, and Chiefs, should be elective and should be limited to two terms, of five years each.

Basic rights; The constitution should protect security, health care, water education, shelter, food and employment, as basic rights of all Kenyans. And this should be sole responsibility of the government.

The constitution should provide for compulsory and free education of both nursery and primary schools.

The constitution should define, and protect education system, Kenyans should have. here, our view is to adopt 7.4.2.3, of form of education. which means, seven years primary, four secondary, two higher, and three university.

Should address the teacher, should address pupil teacher ratio. For both primary and secondary. The current ration 1:54, primary and 1:27 secondary, is not realistic. Our view is should be, the ratio should be, primary, 1:20 and secondary 1:30.

Employment; the constitution should curb the disparity in the remuneration of Kenyan workers. Thus, one worker is paid hectic salary and enjoys a tenureric periodical promotions. While the counterpart works, until he or she retires, without any single promotion. Yet at every point, the two had the same qualifications.

Also the constitution has to address, salary disparity. Where one worker earns, £1,800 annually and the other one earns £180,000 annually.

The concept of quarter system, in admitting Kenyans to education institutions, colleges, and is a mere brain drain. Our view is, merit policy should be used.

Health care; our view is, free medical care for all Kenyans. The concept of cost sharing in our medical services should be

abolished.

The constitution should re-examine, the doctor, patient ratio.

With this, we thank you for the attention, thanks.

Com. Salome Muigai: Please sign there. Maloba Johnstone, it is your turn now.

Maloba Johnstone: Maloba Johnstone is my name, I am a civic education provider, representing Butesero. At the same time, I am a K.A.N.U chairman, West Marama sub branch. I have here, my observation, or what I will need, at least looked into.

I would like a constitution, at least to have an Act or a clause, to outlaw, marriage by eloping. Here I have a girl, she is taken care of as a child by parents while young, up to the stage of eloping. Here parents seem to shade their responsibilities to this girl, probably thinking it has been taken by the husband and his parents. To an adverse, the boy was not marrying, but just trying for about a month, it turns out that the girl is not married, and that she is to go back to her parents, where she had already lost the sense of responsibility by her parents. Here, this girl's rights of belonging, are ready infringed and has no Act of taking the boy to court of law.

During her one month's stay, I am coming up with, I am just giving you reason why I think, but I have good results out of this. So, you see, the results of this, of what I am talking about is that, the girl, the channel of inheriting is infringed by this, will be illegal marriage. Now, if we outlawed, marriage by eloping, most likely, so that, first you will leave me just to finish, because I am going step by step.

Com. Salome Muigai: Go on.

Maloba Johnstone: Because I had not completely what, so that I come out with my, okay. During her stay with this boy, during the one month's trial staying as an eloped girl. This lady, most likely has got herself pregnant, she is pregnant. And by the time she is chased away by this boy, the girl is already pregnant. The results; the girl's channel of inheriting is infringed by this, will be illegal marriage.

Two, the best care, an offspring gets from happy parents, will miss on this she will be getting from this emergent marriage.

The girl is now dubbed second hand, and you see the moral of the girl is already infringed.

Four, her offspring may end up a street boy or girl.

So, you see, these ones are my points supporting, why we should outlaw, marriage by eloping.

How do we prevent this? People marrying, out to sign a binding document. Soon as they think of it, dowry can even come later, as per the document.

There should be an Act, completely outlawing marriage by eloping. That is my first observation, as that one goes.

The second one is just, the electorate and their representatives. Here it is just a statement that I would like done. Some representatives become a nuisance, soon as they have been elected. We should have a clean Act, allowing the electorate to pass a vote of no confidence, thus the percentage, at least, if we got a clause somewhere in our constitution, which stipulates that, if you become unhappy with your M.P or your Councillor or whoever you have elected to parliament, you prove, you gather a certain percentage of people, the electorates. And then host the M.P or the Councillor, that one will be at least good. I don't have much.

Com. Salome Muigai: Thank you for your views, Johab Maero.

Johab Maero: Kwa majina yangu, naitwa Johab Maero Ashika, na mimi nakuja mbele ya commission hii kwa niaba yangu.

Kitu cha kwanza na tena na commission, mimi ningependelea yafuatayo.

Kama mimi mwanaraia wa Kenya, serikali ambayo iko kwa mamlaka, ambayo imechaguliwa. Ya kwanza, lazima ijuwe mwananchi ni nani. Hiyo ndio maoni yangu. Lazima serikali ijuwe mwananchi anataka nini, ni kitu gani mwananchi anataka.

Kitu cha pili, mwananchi ambaye ndiye anaweka serikali katika mamlaka, ni kitu gani serikali inataka, ama inaweza kufanyia huyu binadamu ama mwananchi wa Kenya. Mara nyingi sana, serikali imesahau mwananchi. Kama naweza kumpa tu example ya hapa juzi. Watu wanateseka kufuatana na malaria ama ugonjwa, serikali imesahau kabisa, ni ikisikia ati kwa sababu watu iko ugonjwa mahali fulani ndio serikali inakimbilia. (**Interjection**)

Com. Salome Muigai: Tafadhali tupe mapendekezo, wewe mwenyewe ungetaka kuona nini?

Johab Maero: Sasa ningetaka ya kwamba, serikali ambayo inachaguliwa, itambui binadamu ama mwananchi.

Serikali ambayo iko mamlakani, iwe ama a president awe katika ofisi kwa term mbili. Ya miaka tano.

Na katika ofisi, ikiwa ako mamlakani kwa hiyo miaka tano, mwananchi ambaye amemchaguwa, waite elections ya maoni, mwananchi aone, ama apige kura, ati serikali inaendelea mzuri ama mwenye ako mamlakani anaendelea vizuri ama ako namna gani. Kwa sababu ni mwananchi huyu, ndiye alimwandika katika hiyo ofisi.

Kuchaguliwa kwa officers, kama judiciary. Hiyo judiciary, iwe independent, iwe tu peke yake. Ipewe mamlaka ya kuchunguza, kwa sababu hiyo, ndio mwananchi ambaye anafinywa, saa ingine na maneno hapa na pale. Anaweza kukimbilia. Lakini iko interference nyingi, kufuatana na hiyo office. Uwezi enda kwa ofisi ama kwa mahakama, wewe kama common man, halafu usikilizwe kwa njia nzuri. Na hiyo inatajikana, hiyo ipewe uhuru, mwananchi apewe uhuru ya mwenyewe kujitambulisha, na ku represent maneno yake, katika mahakama. Yangu ilikuwa ni hiyo peke yake.

Com. Salome Muigai: Asante sana, tafadhali jiandikishe. Enoch Musungu.

Enoch Musungu: Kwa majina naitwa Enoch Musungu, wa Salvation Army. Yangu ni machache.

Ningependa serikali ambayo inakuja, iwe parliamentary system of government, ambayo tutakuwa na prime minister, kutoka kwa chama ambacho kitakuwa na Wabunge wengi, Bungeni.

Ningependa, raisi asiwe juu ya sheria. Sheria iweze kufanya kazi hata kwa raisi, akikosa aweze kufungwa kama mtu mwingine yeyote.

Raisi asiwe Mbunge.

Raisi aweze kumteua makamu wa raisi na ma ministers, lakini asiwe na uwezo wa kuwaachisha kazi. Hiyo uwezo iwachiwe Bunge.

Raisi aweze kudumu kwa miaka mitano, na akienda zaidi, iwe miaka kumi, ikiwa alikuwa anafanya vizuri. iwe miaka kumi na akito kwa ofisi, asilipwe kitu baada ya kazi.

Ningependa sheria, ifanye kazi kwa mkubwa, hata kwa mdogo, kwa sababu, sheria ya sasa ifanyi kazi kwa mkubwa na kwa mdogo. Mtu mkubwa akiiba kitu, hachukuliwi hatua, lakini watu wadogo, wanaumizwa sana.

Bunge; ningependa katika Bunge, speaker awe yeye ndiye ana uwezo wa kuvunja na kusongesha Bunge, sio raisi. Kwa sababu yeye ndiye anashughulika na mambo ya Bunge.

Ningependa Bill zinazopitishwa Bungeni, ziwe signed na Attorney General, mkuu wa sheria. Raisi asi sign kwa sababu raisi ajui

sheria, mkuu wa sheria ndiye anajua sheria. Kwa hivyo Bunge inaweza pitisha kitu mbaya, na raisi anaweka mkono. Hiyo, ninaonelea ni vibaya.

Ningependa Kenya Gazette, ambalo linatangaza mambo ya serikali, liweze kuuziwa kila mmoja, liweze kupatikana kama mafazeti ingine, tunavyo yapata.

Na Mbunge aweze kudumu kwa miaka mitano, na akienda zaidi iwe miaka kumi. Na arudi nyumbani, hata asipewe u chairman mahali popote. Kwa sababu kuna watu wengi wanataka kazi.

Ningependa Bunge isizugungumzie mambo ya mishahara yao. Tuwe na special commission ya kuzungumzia mishahara yao. Kwa sababu wanapoenda hapo, wanazungumzia mishahara yao, wanaongeza zaidi, mpaka uchumi inaharibika.

Bills of Rights; ningependa, koti isiwe na uwezo wa kuweza kuweka mtu, ati anaenda kunyongwa. Mtu asinyongwe, bali afungwe maisha.

Uhuru wa kuabudu; ningependa iwekwe limit. Kwa sababu tumewachilia hiyo uhuru, na tunapata makanisa mengi, hata saa hii watu wanaabudu shetani. Ambayo tunakuna ma accident mingi sana inatokeana na uhuru wa kuabudu.

Na upande wa chang'aa, ningependa kusema chang'aa iwe halali, na hiyo chang'aa inapokuwa halali, isiuzwe, iwe halali, watu wakunywe bure, na ukipatika unauza ufungwe miaka saba.

Mambo ya mashamba; yawachiwe wazee wa kijiji. Hiyo board itoke kwa D.O, D.O asiwe mwenyekiti wa Board, aji mambo ya mashamba huku. Hiyo mashamba irudi kwa wazee, wazee wenyewe wajiadiliane mambo ya mashamba na vile inaenda. Na hiyo title deed iweze kupatikana kwa kila mkenya.

Ningependa tena mambo ya mashamba; katika Katiba yetu, tuwe na kitu tunaita Jubilee. Hili miaka fulani, mashamba inarudi kwa serikali, serikali inagawia watu, kuingana na hesabu ambayo iko. Kwa sababu tuna watu wengine wana mashamba, acre elfu mia tatu, na wengine hawana kama mimi ninavyozungumza hivi. Kwa hivyo mimi ni mkenya.

Upande wa elimu; ningependa, serikali iweke elimu kwa watoto wale ambao wazazi wamekufa kwa njia ya ukimwi. Kwa sababu hii ni chango la taifa nzima. Hao watoto wasomeshe kuanzia nursery mpaka form four, mpaka university, hata ng' ambo wapelekwe.

Mishahara ya walimu; ningependa isiwe ni kitu ambayo inajadiliwa kila mara. Katiba iweke mishahara ya mwalimu inasongeshwa baada ya mwaka mmoja percentage fulani, walimu wanafanya kazi nyingi. (**Interjection**)

Com. Salome Muigai: Tafadhali malizia.

Enock Musungu: Ninamaliza, namaliza.

Kwanza hapo kwa walimu, nataka mwalimu wa nursery awe analipwa na serikali. Kwa sababu tunaambiwa elimu ni ya bure, nursery tumewachiwa.

Local government; Assistant Chief na Chief, waende transfer. Hao watu ni kama civil servants wengine. Wapelekwe transfer na *maguru* wapewe mishahara.

Police; police wasiwe ni police force, bali wawe police serving. Siku hizi tuko na police force, hata hawawezi kusaidia wewe, wanakuumiza tu. Hawa watu wa army, wawe na kazi ingine ya ujuzi, ambayo wanaweza kutekeleza na kuingiza pesa kwa serikali. Asante mengine mtasoma.

Com. Salome Muigai: Stanley Muka.

Stanley Muka: My name is Stanley Muka, I am a retired civil (**Interjection**)

Com. Salome Muigai: Mu?

Stanley Muka: Muka, M-U-K-A, a retired civil servant, both locally and internationally.

General remarks, the constitution as a document, should be respected, and to me a constitution is a sacred document which should not be tampered with. And once written, it should remain and serve for a long time.

On that one I suggest that, if the two term presidency is upheld, that part should not be changed at all.

Constituencies; my humble opinion is a constituency should be fixed, and not just created at randomly. I am thinking personally that 200, 250 will be enough constituencies to serve Kenya.

Parliament; the original constitution, majimbo constitution, we had two houses, senate and the house of representatives. I suggest, that the two houses be re-introduced. A senate, personally I will think the best way for senate, will be to use tribes, so that tribes can be recognized rather than ignored as we ignore them now.

There are members who are nominated to parliament. my suggestion is this should be abolished. There is no need to appoint anyone at all in the house.

Qualification of M.Ps; I think ability to read and write, and speak in English and Kiswahili, should be what is wanted. If education is wanted at all, school certificate is enough. Degrees are not wanted for parliament work, the ability to practise politics, to talk convincingly, is what is wanted in parliament.

Presidency, a very important institution, need to be respected. It's job should be to coordinate, the activities of the government. And be a (Inaudible) or a centre of gravity.

Ministries should not be created in the Office of the President at all. Ministries should be in their own line, and if any ministry is in the Office of the President, they should not help to coordinate work of other ministries.

So I say, the hold of the presidency should be two terms of five years each, as it is now.

While occupying the Office of the Presidency, Ministers, Assistant Ministers, top civil servants, Permanent Secretaries, D.C, P.Cs, should not be allowed to practice business. They should concentrate on employment, if they want to do business, leave public work and go to business.

Top appointment should be vetted in Parliament, where the president has to appoint certain people, commission of police, what Armed Chief defense should be, should be appointed by, should be vetted by the parliament.

Cabinet; I feel cabinet should be trimmed in the new constitution, and the constitution should spell the number of ministries we need. Personally I think, eleven to 15 ministries, will serve the government. And they should be, maybe 15 – 25 Assistant Ministers. We don't need a parliament that is full of ministers all the time.

On Assistant Ministers; I think they should be upgraded and called Vice or Deputy, in which they can be deputize, if the minister is away.

Judiciary, the parliament and the executive or the presidency, should indeed be separate. Each with its own role to play, each independent, that coordinate to serve the same government.

The new government should certainly emphasis aspiration of those powers

Public Service Commission, I think should be strengthened, and appoint people and promote them to the highest possible level.

Even need be the D.C, the P.C should be appointed by the Public Service Commission, they are civil servants. If they are to be appointed by the president, then the Public Service Commission, short list three names which should be represented and then from there appointments made.

On land; I feel that, the Commission of Land or whoever is empowered to dish our land, should be the only person dishing land, nobody else, no other authority should dish out land. And he should also prepare due documents alone without anybody else, not even the president is to issue land.

Human rights; I consider education and health, two top human rights. education should be up to a certain level, should be decided, universal primary education. maybe standard one to standard eight, should be mandated, and easy to be done. and means to ensure that they are carried out as done. same with health.

Cost sharing, I begin to see that there are many people who cannot even afford the cost sharing, no matter how much little money they have to pay. So I feel, that they should be free service.

Com. Salome Muigai: Your last point Sir.

Stanley Muka: Freedom of press, freedom of human rights should be upheld. Can you give me a minute to conclude?

I wanted to mention something in retirement. Retirement age should be increased from 55 to 60. 55 being optional, 60 being mandatory, and that anybody who is on retirement, should get a better benefit, a thousand shillings is a minimum. I think less than a thousand shillings for people who served a long time ago, and the shilling was strong, even less than a thousand shillings is not valued. There is no need in fact to be on a rosta for retirement, when you are getting less than a thousand shillings. You said I can leave this view, it is written in the exercise because I haven't finished.

Okay thank you, I will conclude by saying, the constitution no matter how beautiful it is written, no matter when it is written, it is the people who are going to implement, that will matter. If they want to tamper with it, they will tamper with it. so we must have a clause which means that, no tampering with the constitution once it has been done, for the sake of the old. Thank you very much.

Com. Salome Muigai: Francis Shibola

Francis Shibola: Kwa jina langu naitwa Francis Shibola Shingoro, ninasonga mblele ya tume, kuwakilisha chama changu cha Development Help Group.

Kwa upande wangu na maoni ya wenzangu wote, wanaonelea kuwa, nataka kama serikali ingelipendelea na tena maoni yetu, huwa tuna register kila mwaka, yaani tunajiandikisha kila mwaka, lakini usaidizi wowote huwa hatupati. Kwa hivyo tunaomba tume itusaidia, ikiwa itawezekana, serikali inayokuja wakati mwingine, iwe pesa ikitoka, iwe mkitusaidia kitu kidogo. Watu wetu wapate maendeleo na kusomesha watoto, kuwapeleka katika skuli.

La pili ni hivi, tungeliomba tume, watoto wetu wakiingia katika nursery mpaka standard eight, huku kwetu huwa tunangaishwa sana. na upande wa malipo kila mara watoto wakienda skuli. Tunalipa school fund, tunalipa nini. (Interjection)

Com. Salome Muigai: Unapendekeza nini?

Francis Shibola: Mapendekezo yetu tungelionelea, afadhali serikali na tume ingetuwachia tu, tulipe school fund peke yake. Ni hayo tu, sina mengine ya kuendelea nayo.

Com. Salome Muigai: Naomba tuwe na mkutano mmoja, kwani tuna nasa hayo maneno yote yenye inakuja kwa kanda ya kunasia habari. Kwa hivyo kukiwa na kelele, pia hizo kelele zinaswa. Na wakati tutakapokuwa tukisikiza vile watu wa Butere walivyosema, tutakapo kuwa Nairobi, hizo kelele zitatutaliza, kwa kuwasikia ile maneno yenye mlituletea. Kwa hivyo tafadhali naomba, tujaribu kutulia, ndio tusikilizane. Yusuf Makhokha.

Yusuf Makhokho: Kwa majina ni Yusuf Makhokha, ningependelea kutoa maoni yangu kuhusu wezi. Ningependa kutoa maoni yangu, serikali haingekuwa inakubaliana kutoa bond kwa mwizi. Suspect, ndio anatakikana apewe bond, kwa maana anashukiwa tu ni mwizi, apewe bond awe nje.

Inginge, sisi tunalia uchumi umesorota, ambapo serikali yenyewe ndio inatumia pesa nyingi, kwa kulipa wizara nyingi. (Interjection)

Com. Salome Muigai: Unapendekeza nini?

Yusuf Makhokho: Ipunguzwe.

Com. Salome Muigai: Kutoka ngapi mpaka ngapi?

Yusuf Makhokho: Iko ngapi saa hii?

Com. Salome Muigai: Ungependa ziwe ngapi?

Yusuf Makhokho: Ningependa ziwe kumi na nane.

Com. Salome Muigai: Jambo lingine, ama umemaliza?

Yusuf Makhokho: Jambo lingine; sisi tuko na utamaduni ya Kiluhya, tunafaa tupewe barua ya kungoja ugeni, tusiwe tunauziwa barua.

Com. Salome Muigai: Hizo ni barua gani?

Yusuf Makhokho: Za kunini, tukiwa na sherehe, uwa tunaenda kwa O.C.S kupata barua na wanatuuzia, badala watupe bure, kunugoja ugeni. Nafikiri hiyo inatosha.

Com. Salome Muigai: Asante sana, jiandikishe pale tafadhali. William Anyanga.

William Anyanga: Yangu ninataka kuchangia, ni kuongea juu ya Mbunge. Jina langu ni William Anyanga Makunda.

Mbunge afanye kazi, kuanzia Juma tatu mpaka Ijumaa. Kuanzia saa nne hadi saa tisa.

Mshahara wa Mbunge huyo, iwe shilingi elfu hamsini.

Mbunge ni mzazi, ni mchungaji na ni mzaliwa wa Kenya, asipew e ruhusa ya kumeza mshahara ya watu mia mbili au mia tatu. Kama retired, orphans, widower, waliacha kazi kwa lazima, wale waliwacha kazi kwa lazima.

Mbunge achaguliwe na raia, tena awachiwe raia kumfuta, na kuwacha kuchagua mwingine. Hata hiyo ifanyike tu, pia na raisi. Raisi kama amechaguliwa na raia tena, wawachie raia wamfute. Ningekuwa na mengi ya kusema lakini, mengi nilikuwa nimeandika kwa Kiluhya, sasa nitampa tu huyu andike.

Com. Salome Muigai: Umeandika hapo kwa Kiluhya? Elphas Amolo, (Inaudible).

Elphas Amolo: Kwa majina ni Elphas Amolo Linyerera. Ningependa kuchangia mjadala wa administration.

Pombe ya chang'aa kwelie serikali imekataa, lakini ya kwamba, ni maajabu sana, kuona ile manyumba yenye anafanyia kazi, watu wa chang'aa ndio wana sponsor hao. Sasa chang'aa itakuwaje isimame. Kwa hivyo mtu kama Assistant Chief na Chief, wanastahili wawe na transfer.

Ya pili, Chiefs na Assistant Chiefs, wanachukuwa mavasi yao ya serikali, kuwa silaha ya kuumizia raia. Unaweza kumpata Assistant Chief, anajua tu huyu ni mwanamke wa mtu, lakini anamfanya kuwa rafiki yake. **(Interjection)**

Com. Salome Muigai: Unapendekeza nini?

Elphas Amolo: Ninapendekeza tu hiyo mjadala.

Com. Salome Muigai: Ungetaka kuona nini ikifanyika, ungetaka tubadilishe nini, ungetaka sheria na Katiba ibadilishe nini?

Elphas Amolo: Upande wa Assistant Chief, akipatikana na makosa kama hayo, anastahili afutwe kazi. Sina mengi, hayo ni yangu tu, niko na memorandum ile nitapeana.

Com. Salome Muigai: Asante sana, ipeane pale. Duncan Juma.

Duncan Juma: I am Duncan Juma, and my views are; **(End of tape)**

To be restored. And the chairman of this particular KACA ,should have some legal knowledge and not appointed by the president of the day, but by the parliament.

All senior civil servants like the Permanent Secretaries, Provincial Commissioners, Parastatal Head, should be vetted by the parliament and not the president.

All ministers and their assistants, plus their Permanent Secretaries, should be professionals with relevant professional qualifications and not necessarily M.Ps.

There should not be a point of cost sharing primary education, and if need be, and the primary education, there should be a fee which should be levied, and should be uniform to all public schools.

The judiciary should have its independence.

The appointment of the C.J and the Attorney General, should be by a parliamentary committee, in charge of public service.

The president should not be above law, and should be convicted in a court of law, whenever he commits a crime, just like any other citizen.

And government vehicles should only be used on official duty, and should remain under government custody, that is in the government security.

All vehicles should be kept at Police Stations, that is the government vehicles.

The constitution should be able to state, and exact date, when the parliament life ends, and not be in the president's hand.

All Commission of Inquiry, should be compelled to by law, to make the finding public, and there should be a time duration, when this should be done so.

And I also recommend that KACA be fully empowered to prosecute, and KACA should also be attached to the parliament, not in the Public Account's Committee and P.I, to follow up cases of corruption and embezzlement of public funds.

And the presidential immunity from prosecution, should be done away with, so that the president can be sued for any misconduct. This will make them more accountable.

The public order Act should be reviewed and Kenyans be allowed to freedom to drink their traditional brews like Busaa.

And Kenyans should also be allowed to organize meetings, and meet without police interference.

Before any such is done by police, the policemen should be able to produce a search warrant, and this should be signed by the chief and the sub chief, and they should also be accompanied by a village elder for identification purposes.

And anyone who wants to invest in a country should do so freely without a lot of this red tape.

The media should be liberalized in a way that, anyone wishing to broadcast, should do it freely, and it should not be owned by the ruling party in power.

The position of Assistant Chief, should be scrapped and instead, the Village Headmen, should be empowered to deal with this village issues, in conjunction with the Chiefs and the D.Os and they should be paid, there should be some salaries to them.

And the chairman of the Land Board should not be a foreigner, but a local person, that is, the D.O should not be the chairman of the Land Board, because he does not know what has been happening in the local area.

And corrupt civil servants, if found to have a case to answer, should relinquish his public office, until the verdict is reached.

Any civil servant found guilty of embezzlement of public funds, should be forced to return back the money and dismissed from his duties.

And there should be a limit on land possession or ownership. In that, beyond that particular limit, the rest of the land is supposed to be repossessed by the government, and given to squatters. (**Interjection**)

Com. Salome Muigai: Is that your last point?

Duncan Juma: No.

Com. Salome Muigai: Then give me the last one.

Duncan Juma: There should be one man one job situation, so that everybody gets a share on the government resources.

Com. Salome Muigai: Inaudible.

Two, you said that, you have talked about village elders. Are village elders men or they women or are they mixed, what is it, tell the situation.

Duncan Juma: The situation is that, we have women and men.

Com. Salome Muigai: Okay, number of acres?

Duncan Juma: A maximum of a thousand acre, beyond a thousand, the rest of the land is supposed to be repossessed by the government.

Com. Salome Muigai: That is his opinion, each of us will have a chance to come and give his own views, thank you very much. Bernard Chema, a student, followed closely by Dolphin Okotchi.

Bernard Chema: On behalf of the school, I present the following. (**Interjection**)

Com. Salome Muigai: The name?

Com. Salome Muigai: The name is Bernard Chema.

Bernard Chema: The president should not be above the law. This is to reduce the chances whereby he has mistakes and not judged accordingly or immediately.

Number two; free primary education and reduction in secondary school fees. This is due to the economy of Kenya, whereby some parents cannot afford to educate their children, because their earning is not enough.

Point number three; the position of the Provincial Administration, should be elective. This is to have a representative from each tribe or rather community.

There should be also free education to the disabled children, but should depend according to the parent's ability.

Then, the ministers and other senior government members, should be reduced. Number five.

The ministers and other governments, their salaries should be reduced.

The government should deal strictly with corruption within the leaders.

Money used on AIDS control ways, should be increased.

Then, for somebody to contest for presidency, he should have academic qualifications. Hereby I mean, he should have or she should have a degree.

Then the president post, should be reduced to create job opportunities to other many unemployed people, but learned.

Birthrate should be controlled. Every Kenyan must have a maximum of three, and for extra, he should be or the parents should be taxed.

Candidates contesting for seats, should not use large sums when campaigning to citizens. This results to more cases of corruption.

Corporal punishment in schools should be allowed, but with strict guidance. This is to remove the Act of heavy punishment, whereby a student does the punishment for two hours, hence misusing the time.

Then, distribution of land, especially to squatters, should be strictly looked into, rather than sparing of land for no apparent reason. And yet many landless squatters are within.

Com. Salome Muigai: Inaudible.

Bernard Chema: The buying and selling of local breweries should be allowed, but under license and the sellers should be given a specific time of selling these breweries.

Then lastly, harassment from the police, should be avoided. And anybody to be taken in a custody, should not be treated miserably, thank you.

Com. Salome Muigai: Thank you. Dolphin Okotchi

Dolphin Okotchi: Thank you, my names are Dolphin Okotchi representing the Lunza sub location youth group. I am representing the right of a girl child.

Inheritance; girls should have a share to inherit land, and the government should get involved to see to it that, all girls should have a share to inherit land. This due to lack of inhering land may arise to problems such as; the girl may end up getting married to families which are poor, and yet back at their home they had big lands, but they didn't have a share to inherit. Or, the family may give birth to only girls, and the parents of the girls may see to it, it is better to sell the land, then they end up suffering, yet the girls are there to inherit the land.

Com. Salome Muigai: Excuse me, are you a student here, so why didn't you have a girl student. Give the name as a girl student, they are talking about their rights.

To my second point, education. the girl education should be supported, for instance, the schools should be supplied with enough facilities, such as the facilities used in the laboratory. This is to encourage the girls to be able to learn more science technology which can improve the country

My third point, the tradition should be weakened, such as inheriting women. This is so to prevent the spread of AIDS, or the girls being forced to marry at a tender age. This is to reduce their chance to achieve greater things. Those are my points.

Com. Salome Muigai: Frida Wabuko.

Frida Wabuko: Frida Wabuko represents Butesero na Kenya Women Finance Trust, Haki and Kimusingi.

Maternity leave; akina mama wapewe maternity leave ya miezi nne, na baba mwezi mmoja, wakiwa na full pay on government

job.

Private sectors; akina mama wapewe three months leave, baba one month leave, with full pay.

Working force; scheme farms. Let big shambas be spared and be cultivated to feed the whole nation. While mamas are busy giving birth and nursing the young ones, let the babas be busy tilling the land.

Number of children for Kenyans; now that Kenya has a bigger number of very poor people na maintaining it is harder than the rich. Let the government give out the specific number of children for each couple.

Com. Swazuri: How many?

Frida Wabuko: Roughly four.

Banks; service charges in banks are too high. Minimum amount to give interest is too high. Let them be reduced. Loan interest are a threat, yet interest to give to customers, on savings and fixed account, are too low. Let there be banks, to cater for small and poor traders.

FIDA; FIDA is a body that fights for poor ladies, let them be from a level of a division, to allow all women, to reach them with their problems.

Madawa; madawa ya genetics, yatolewe kabisa kwa markets, tuwe na originals peke yake.

Madktari u charge very high fees for treatment. We would like you to help us have them reduced.

Madawa ya kulevya yapigwe marufuku kabisa.

Salaries should be discussed by unneutral body.

Mengine nimeandika na mtasoma baadaye, asante.

Com. Salome Muigai: Asante sana mama, Thomas, tulipata msichana wa student, tafadhali njoo, do you have something to share with us? They have gone to bring what, the girl? They are not ready? Okay, Thomas Nambwaya.

Thomas Nambwaya: Kwa majina naitwa Thomas Nambwaya Munyaku, nimekuja kuwakilisha chama cha Avaremerwa Self Help Group, ambacho kimekuwa na mambo machache, kuhusiana na raia.

Na, raia ni Mkenya aliyezaliwa na Mkenya ambaye asili yake, ilikuwa hapo tangu kuchorwa kwa dhamani ya Kenya. Nikujieleza wazi wazi, nikujielezea wazi wazi, kwa kupitia ukoo wake. Yaani, raia awe amejelezea wazi wazi kupitia ukoo wake.

Wawe na kitambulisho kinachoonyesha yeye ni mkenya halisi.

Usalama na ulinzi; ni lazima wakubwa kwa wadogo, kufuata amri, zilizowekwe kulingana na haki za binadamu.

Bunge liwe na mamlaka ya kutangaza vita.

Muundo na aina ya serikali; tuendeele na muundo wa waziri mkuu, ubunge na majimbo. Na Bunge liwe na mamlaka ya nchi.

Upande wa kuajiri; mishahara ya waziri iwe elfu thelathini, hili kuwezesha watu wasio na kazi kuajiriwa.

Mwenye kuajiriwa awe raia wa Kenya, sio mgeni kuajiriwa na kuna watu ambao wanaweza kufanya kazi hiyo.

Kila aliyeajiriwa afanye kazi moja.

Kila mtu aliyesoma, aajiriwe kulingana na masomo, kwa kupunguza umasikini.

Masomo; serikali isomeshe watoto kutoka nursery, hadi shule ya upili, na wazazi wasiulizwe kitu chochote kulingana na gharama ya shule.

Nikimalizia, matibabu; hosipitali za serikali, haziitaji kulipiza wagonjwa gharama. Kwa sababu, gharama za hosipitali huwa zinagharamiwa na serikali. Na ni hayo tu ambayo nimekuwa nayo.

Com. Salome Muigai: Asante sana. tafadhali tukiwa na mzee, mzee kabisa wa miaka themanini, nishulishwe kuwa yuko hapa, nitampa nafasi ya kwanza, tukiwa na mtu mwenye ulemavu, nijulishwe yuko hapa, nitampa nafasi ya kwanza, niwajulisha before vile itafanywa, niletee jina lako. Kukiwa na mama mzee nitampa nafasi ya kwanza, kukiwa na mama mja mzito nitampa nafasi ya kwanza. Lakini lazima nijulishwe tafadhali, kuwa watu hao wenye wanaitaji nafasi za kwanza, mbele mbele. John Wendebwa, or Wandabwa.

John Wandabwa: Majina yangu ni John Leornard Wandabwa, ambaye ni mkulima na mstaafu kutoka kwa serikali yetu ya Kenya. Waheshimiwa commissioners, nimeona nimetaabika kidogo, kwa sababu nilikuwa nimeeka hii, nikitara jia kwamba nitajieleza, sijui nitafanya aje lakini. (**Interjection**)

Com. Salome Muigai: Una dakika tano, ikibido sana, itafika nyingine moja.

John Wandabwa: Asante. Upande wa vyama vya kisiasa, ningependekeza tuwe na vyama vine peke yake. Kwa sababu vyama vingi vinaleta ukabila katika Kenya.

Ningelipenda pia, mabadiliko katika kupiga kura; naonelea ya kwamba, umri wa miaka kumi na minane, watu hawa wengi wao wangali katika shule, na kwa hivyo naonelea, umri huo uwekwe, uende mpaka miaka ishirini na moja.

Miaka ya kuingia kwa Bunge; ningependa iwe miaka ishirini na tano.

Na ningelipendekeza pia, kuwe na senate katika Kenya, na watu ambao wanafaulu kwenda kwa senate wawe na umri wa miaka hamsini na tano.

Mishahara ya wabunge wetu; naonelea ya kwamba, wabunge wanalipwa kutokana na pesa za raia, na kwa hivyo, ningelipendelea wao pia, Public Service Commission, iwe ikichunguza mishahara yao, na sio hao wenyewe.

Upande wa elimu; naonelea ya kwamba elimu tunajidanganya wakati huu wenyewe tukisema ya kwamba, elimu iwe ni ya bure. Ningelipendekeza kwamba elimu, kuwe na kiwango fulani, cha school fees, ambayo inatotelewa, hili serikali iwe na uwezo wa kujua ni kiasi gani kinafaa. Hili vifaa vyote vya shule viweze kupatikana kwa uraisi, kama chokaa, vitabu, vile tulikuwa tukisoma sisi wengine hapo mbeleni. Ilikuwa nikuenda shule na kupata kila kitu kiko tayari. Kuliko wakati huu ambao mzazi anaambiwa, kwenda kununua kitabu ni shilingi mia tatu, ni shilingi mia nne, na hali elimu inasemekana ni ya bure. Mimi naonelea kama hiyo haitatusaidia sana.

Hapa naona kama, kuna mambo ya watoto ambao wako barabarani. Watoto hawa ambao wako barabarani, ni sana sana kwa mambo, kwa sababu ya umasikini, na pengine wazazi kutojua na kutojali. Na ningependekeza kwamba, mila zetu kama kwa mfano Wabaluhya, mtu akidunga msichana mimba, yeye anakuwa ndiye mwenye mtoto, na anachukuwa kila uwezo wa kumlea mtoto hadi awe mtu mzima. Sababu hiyo imeanza kuwachililia mambo ya kimila, imefanya sasa watoto wanatupwa ovyo, na watoto ambao wako barabarani ningelipenda, kamati iundwe, ya kuchunguza kwanza, kujua watoto hawa wamepatika vipi barabara, hili waweze kuchukuliwa na kupelekwa mahali panapohitajika. Kwa sababu, watu wengi saa hizi, wameanza kutengeza manyumba mengi na mambo mengine mengi, kupata pesa kwa wahisani na kadhalika. Na watu wengine wameanza kutupa watoto wao, kusudi hili wachukuliwe na vyumba vya kusaidia watoto, hili walelewe watoto bila gharama yoyote.

Mashamba, mashamba ningelipendekeza kwamba, mtu mmoja asiwe na zaidi ya hekari mia moja. Na kama ni kwa biashara isiwe zaidi ya hekari elfu kumi. Nafasi hiyo, mashamba ambayo yatapatikana, yataweza kuwasaidia watu wasio na mashamba.

Haina haja ya mtu kukuwa na mashamba mengi katika Kenya, wakati mtu mwingine hana hata acre moja, na mtu mmoja ambebania, dunia mzima ya mashamba.

Mambo ya security, ni jambo la kustaajibisha sana, waheshimiwa commissioner, kuona kwamba, polisi hawana vifaa ambavyo wanaweza kutumia, utakuta gari la polisi linasukumwa. Ni jambo la mzaa kuona, gari ambalo linaenda kufukuza mwizi linasukumwa. Polisi wapewe vifaa vinavyofaa, wapewe mishahara inayofaa, hili wasiweze kuongwa kwa uraisi. Wapewe pia nyumba zilizo mzuri.

Msaada wa sheria; ningependekeza, Law Society of Kenya, iweze kuwa na mpango fulani, labda kama ule wa National Hospital Insurance Fund. Ambako, wananchi wanaweza kuchangia kiasi kidogo, kwa muda, hili shida ikipatikana waweze kusaidiwa.

Na pia katika serikali, itafute njia ya kuweza kuwa na njia yoyote ya kuweza kuwasaidia wale kabisa hawawezi kujiweza kusaidiwa katika hiyo.

Pombe yetu ya kienyeji; mimi napendekeza kwamba pombe ya kienyeji irudi vile ilivyokuwa zamani, lakini isiwe ya kuuza. Iwe vile wazee walikuwa wankunywa zamani. Wazee walikuwa wanatengeza pombe yao, na wana muda wao wa kunywa. Kwa sababu ikianza kuuzwa tena, wataanza tena kuchangia mambo mengine machafu ya kufanya watu kufa. Saa hii tunajaribu kujidanganya kwamba tunazuia pombe, lakini watu wanatengeneza usiku, wanatengeneza watu wanakunywa wanakufa. Naonelea lazima pombe iweko, hili watu wasiangamie.

Retirement; after retirement, the retiree should be give adequate benefit, and not be allowed to be employed, through contract or appointment. For example, a senior retired civil servant in the government, is appointed to the chairman of a different non governmental body, the chairman, and we have people who are not employed.

Okay, last; I think this is the last commission, and the one I have participated in. but in Kenya we have been having a lot of commissioners that have never produced what they have been doing. And I think this one because, most of the commissioners here, I think they are learned friends. So I think what we are trying to do here, let us please get it working. We have a lot of commissioners who work for commissions, that has been taking places, and we have been not knowing clearly, what really expired, they have concluded them, and we have never seen them concluding their work. So this one please, do that. Thank you.

Com. Salome Muigai: Thank you. Livingstone Makura.

Livingstone Makura: Kwa majina naitwa Livingstone Makura, na yangu, point ya kwanza iko kwa mambo ya mashamba.

Shamba, walifanya, waliwapa watu mashamba 1963. ningependelea shamba ifanyiwe review. Watu wamekaa wengi hawana number. Mzee alifariki, na hakuna mtu amefuatilia, pesa ya kupeleka kotini hawana. Kwa hivyo inatakikana government ifanye review ya mashamba, after 10 or 15 years, vile wanafanya high depart, inasaidia watu wengi.

La pili, ingine; surveyor, ukiwa na shida kwa shamba, upeleke kesi kwa surveyor, mzee atakufa kama mtu bado kutoka kwa surveyor. Kwa hivyo nataka surveyor apewe course ya (Inaudible). Hiyo itakuwa inasaidia watu kwa maana iko karibu.

Succession; tunataka succession kama mtu amekufa. Apate kutoka kwa Assistant Chief, kwa Chief, kwa DO halafu aende kwa land, apewe title deed. Hakuna ya kwamba aende kotini huku na huku, mtu atatupa pesa nyingi.

Mtu kama amekufa, mali yake, hata kama ni mtoto msichana, amekuwa na wanawake watatu, apewe, hata mtoto msichana apewe. Hapana kusema ya kwamba kijana ndio atapewa, na huyu mama ako na wasichana peke yake, atoke bure, hata msichana apewe.

La tano; nataka, mtu kama, kwa maana wakati tulipewa hii mashamba, wazee walikuwa hawajui shamba ni nini. Watu wanasema, map ilipeleka shamba yangu kwa mwingine. Mtu kama amekaa mahali, akimaliza miaka ile inatakikana, apewe title deed na serikali

Hii watu wa civil servants, wawe controlled zaidi, kwa maana uufisadi nyingi inatokea kwa civil servant, especially police. Nataka mtu akiwa mahali afanye two years, anachukuwa trnasfre sehemu ingine, anakaa mahali, anashika corruption nyingi, anajua vile anakula na waizi, anajua vile anaiba vitu vya watu, corrupt, huyo anatakikana apewe transfer. Especially kwa police, kotini and what and what.

Mtu akipatikana ni mwizi, hapana ya kwamba ameenda kotini, na mali yake ishikwe iuzwe, pesa irudi na serikali, isaidie wananchi.

Katika court; kesi inaenda kotini, mnatembea miaka tatu, nne, kama bado ijakatwa. Inatakikana kesi ikienda kotini ikuwe three months, iwe hired. Kwa maana ikikaa corruption inakuwa nyingi. Mtu anatafuta kulipa rushwa judge, hata karani pia anakulia huko, hata messenger anakulia kwa hiyo kesi. Kesi ikatwe haraka haraka, mtu ule ajue kama ni kufungwa ama kama ni kuwachiwa awachiwe.

Lingine la mwisho, landless; tunasikianga mtu amelelea kama amepewa shamba, kwa squatters. Na huku kwetu kama Butere hatuna forest ya kama ile watu watavamia ndio wapewe shamba. Nataka kwamba, wangetoa mambo ya kutoa shamba, kwa watu wale hawana shamba. Isukumwe mpaka kwa district level, kwa DO kwa Chief, watafute watu hata huku kwetu pia wapewe hiyo mashamba. Hapa kuna watu wengi hawana mashamba. Kwa hivyo inatakikana uridhi iwe countrywide, kila mtu afikiwiwe, hiyo ndio nilikuwa nayo peke yake.

Com. Salome Muigai: Inaudible.

Livingstone Makura: Unajua hiyo Will vile inasemekana ni, inasemekana kwa njia mbaya. Inasema Will, hiyo kitu mnaandika, mmeweka kwa lawyer, ama umeweka kwa koti, na huku kwetu sisi hatujui hiyo kitu. Lakini mtu akiandika local Will, hawataki kuchukuwa. Kwa hivyo ningependekeza, kama serikali inataka isaidie wananchi kabisa, mtu akipewa title deed, na mama aandike jina juu yake. Halafu wewe ukifa, Chief anatoa tu barua ya ku recommend jina ya mzee itoke, ibaki ya mama

peke yake. Hiyo ndio mimi nafikiria namna hiyo, hapo utasaidia. Na pia, government ikubali local Will, kwa maana sisi waafrika najua nikitaka kufa, nitaita Mwaroma ni ndugu yangu, kuja hapa usikie maneno yangu, maanake sema, serikali iamini Mwaroma, kwa maana ndio nimempa maneno yangu, vile mimi naenda kufa. Sio ya kwamba, sheria ifuate ya kwamba,

(Inaudible) ulienda kotini hakuna. Iwe tu ni kitu ya kutoka haraka.

Com. Salome Muigai: Lakini pia unajua lazima kuwe na, sijui kama unaelewa pia lazima kuwe na watu wawili walisikia ukiambia Mware.

Livingstone Makura: Tunasema nikiita, Mware, ni ndugu yangu. Nintaita wengine, nitaita Ibra akuweko, nitaita washaidi wawili watatu wakuweko, halafu nimwambie maneno yangu, hii nikifa, huyu mtoto wangu mkubwa yeye ni mbaye, umpe ule msichana wangu ashike shamba yangu, halafu atampa wengine. Huyu Mwale akuwe, the final person wangu. Asante.

Com. Salome Muigai: Mlale, Mlale Omany.

Mwale Omany: My name is (Interjection)

Com. Salome Muigai: Mwale?

Mwale Omany: Yes Mwale. My name is Mwale Francis Omany. Mimi hayo ndio yangu ya kusema kwa new constitution;

Kwa maoni yangu naonelea kwamba, kiongozi wa nchi kama raisi, ikiwa anachaguliwa kwa mfano Mkoo wa Magharibi, Coast, mdogo wake vice president, atoke mbali kutoka kwa hiyo Mkowa, wasije wawe kwa Mkoa mmoja. Kwa maana, wakiwa kwa Mkoa mmoja, hiyo Mkoa, ndio itakuwa inapata development peke yake. Na ikiwa raisi anakuwa mbali, nchi itadevelop. Huyu vice president atadevelop pahali yake, na president atadevelop pahali yake.

Uwezo wa raisi, vile wenzangu wamesema, nataka ipunguzwe. Ikiwa amefanya makosa, awekwe kwa sheria, asije awe above the law.

Kujaguliwa kwa Wabunge ama Councillors; kwa maoni yangu naonelea kwamba, kuna saa ile tunafanya campaign, tunapeana ahadi zingine tutafanyia watu. Na tukienda uko, (Inaudible). Kwa hivyo ningomba kwa sheria mpya kwamba, Mbunge ama Councillor, ikiwa anakwenda kwa Bunge ama kwa Councillor na afanyi kazi vile anaahidi, electors ndio employers wake. Kwa hivyo wawe na wapewe uwezo wa kumwondoa huyo mtu ama huyo mtetezi kabla ya wakati, sio ati tungojee mpaka hiyo kipindi. Ikiwa apeani services vile inahitajika, inataka iondolewe na wananchi waliomchagua, achaguwe mwingine.

Waziri akifanya makosa, akipewa kazi kama minister, na awe anamisuse public funds, anaweza toa hiyo ya serikali. Sioni ni maana gani apelekwe kwa ministry ingine, kwa maana akipelekwa hii ministry ingine, ataendelea tena kula hizo pesa, na serikali itaendelea kurudi chini sana. kwa hivyo, badala ya kupelekwa transfer kwa ministry ingine, aondolewe, awe demoted, awe kama MP. Na hiyo ifanyike hata kama ni kwa secretaries na viongozi wengine wa serikali.

Hii maneno ya akina mama kuwa equal kwa wanaume, hii sijui hesabu ilifanywa namna gani. Kwa maana, mwanamke awezi akawa equal kwa mwanaume. Na nafikiri ni lugha, hatujapata lugha mzuri ya kutumia. Nataka kama nilikuwa na, kwa hii sheria, ningesema hivi, tuwe na heshima kati ya mke na mume. Lakini si mke awe equal kwa mwanaume. Haitafanyika, na iwezi fanyika hiyo.

Now, kufika kwa wakati wa hii viongozi wa administrators. Kwa maoni yangu naonelea ya kwamba, hii ofisi ya Assistant Chief iondolewe kabisa. Ina exhaust fedha za treasury for nothing. Kwa maana unaweza kupata maneno inafanyika kwa Sub location, Assistant Chief anashika hiyo maneno, inarudi inaingia kwa Chief, halafu Chief inakwenda kwa DO, hii ni ku waste time. Kwa maana, hii wazee, wale leaders, village leaders, ndio wanafanya kazi nyingi sana. and I would suggest, hawa village leaders, wapewe uwezo, ndio wanajua vitu vya villagers, na wao wana deal direct na Chief. Office ya Chief iwe, lakini office ya Assistant Chief iondolewe, they are excesssly (Inaudilbe) because, ile maneno wanafanya tena itakwenda kwa Chief, na itakuwa mzuri. Kwa maana kwa sheria mpya, hiyo office iondolewe.

Tukija kwa maneno ya pombe ya kienyeji (**Interjection**)

Com. Salome Muigai: Una saa moja.

Mwale Omanyoo: Okay thank you. Maneno ya pombe ya kienyeji, mimi ningependelea hivi; hii pombe ya chang'aa watu wanatengeneza na serikali haitaki, na ukikataa ndio watu wanatengeneza hiyo. Watu wapewe uwezo, wale watu wa kutengeneza chang'aa watengeneze chang'aa. Serikali itengeneze industry, ile ya ku disbalance hii pombe ikitengenezwa na hawa locals. Nayo iende kwa industry fulani, iongezwe chemicals, iwe Kenya Wines. Kwa maana sisi hatuna pombe za kienyeji, na sasa tunasema Tusker, Guinness, hii ni pombe inatoka nje, na yetu hatutaki. Kwa hivyo, ningenelea ya kwamba, hii chang'aa wapewe uwezo, watengeneze na tuwe na industry ya ku sterilize hii pombe, nayo iwe pombe ya kina Whisky mzuri, ile watu watakuwa tukitumia.

Upande wa education, corporal punishment should be in schools. (**Interjection**)

Com. Salome Muigai: Hiyo point ya mwisho.

Mwale Omanyoo: Yes. Corporal punishment should be in schools, because, tukiwacha tu namna hiyo watoto, walimu wasije

wakawapunish, we shall have very poor products. Hao watoto hawatajali nini inaendelea. Kwa hivyo ningeomba the corporal punishment iwe kwa schools. Thank very much.

Com. Salome Muigai: Ruphas Mukonasi.

Ruphas Mukonasi: Your honour, they call me, those who know me, Ruphas Sorem Mukonasi by names, and I have the following observations to make;

One; once a president retires, he or she should relinquish, his or her any party position, he or she held prior to the retirement. For this one was evidenced by the founding father of Tanzania. When Julius Kabarage Nyerere retired, but overshadowed Mwinyi, when he remained C.C.M chairman.

Two; for national harmony, a wining party in general election, should incorporate, first runners up in the formation of government, for better governance. This one has been evidenced by the K.A.N.U, N.D.P partnership, which at least so a little improvement in governance.

Three; the state in which Kenya is, where each and every ethnic group is anxious and lusting for power, I suggest to call it, I presume that regional government, would be suitable, just like we had it at independence. When Western region had its Headquarters at Kitale, with Wafula Obuke as his president.

Four; I also concur, with those who propose that Kenya should have a ceremonial president with a prime minister. And be part of it, I want to say here, that teachers should be given lucrative pay, for their normal job of moulding a nation. So that we can control this strike business. Because they are doing a lot of job.

Five; corruption during electioneering time, I propose that political aspirance of any post, may it be parliamentary or civic. Be victimized if found bribing voters, for this leads to electing tycoons, who may not be politically competent. Hence creating poor governance in the country.

And number six, any ruling party, should not influence administration, because this one causes biasness in administration. And it should not influence judiciary, judiciary should be left to be independent. We should have limited number of parties, call it political parties. And the government, if it has to finance any political party, it should finance all parties, including opposition.

Seven which is the last one, you honour, I want to request that the constitution should stop this people in the, our people in

(Inaudible) whether they are government officials or what, banking money outside the country. Because the moment they bank money outside the country, they drain the economy of this particular country. Your honour, I had those few remarks to make, but if I had time I would produce more copies to give you. Thank you very much for listening to me.

Com. Salome Muigai: Thank you, I have one question for you. How can you know the political parties, do you have an idea of what number they should be.

Ruphas Mukonasi: Approximately five will do.

Com. Salome Muigai: Five will do.

Ruphas Mukonasi: Yes. My name is Ruphas Sorem Mukonasi, a retired teacher.

Com. Salome Muigai: Wycliff Mutakha.

Wycliff Mutakha: Yes, I am Wycliff Daniel Osako Mutakha.

Com. Salome Muigai: Mutaka?

Wycliff Mutakha: Mutakha

Com. Salome Muigai: Not Mutaka, Mutakha.

Com. Salome Muigai: Mutakha.

I am a retired High Court Librarian in Mombasa. And with the honour given to me, your honour commissioners, I have the following to submit;

One; I recommend Kenya to have a regional government, with two houses of law.

1. House of representatives, to consist of elected represented members by the constituency.
2. Regional Assembly, with at least a representative or two, per each district in the republic.

This should be headed by a prime minister who should be responsible to parliament, with a ceremonial president, to do the same in any ceremonial function in the republic.

Two, parliament; parliament should have power of making laws. And not to be a rubber stamp to the executive as it is today.

Any elected member should be free to contribute to any motion freely, independently, without any fear at all.

Judiciary should be headed by well qualified personnel, who should be free and judicious, to pass their decisions.

Executive; the executive should not asarb the powers of judiciary and parliament as it is, or any other parastatal body.

Distribution of the national cake; this should be done evenly and according to the district and to the country's years of development, and by the countries censors.

Employment; employment should be done evenly and by the qualification, not on tribal of sectionalism based.

The country security; on country security I would say, the security is a small gadget in the constition, and should have the power they have. not unlike in some other parts, where we find, let's say for example the Aps, they can gang up with. **(End of tape)**

He is not take to court, they make Kangaroo courts, they collect some money, how does the government value from this. There should be a law, where such a person is found, he should be fires, and if possible prosecuted.

Provincial Administration; Provincial Administration I think should, Chiefs and Assistant Chiefs, D.Os and whatever, should be elected by votes of mwananchi.

Minority groups, walemavu and insane, should be at least be accorded some role in the constitution, not just to be left that way. Where you find the Municipalities, City Councils, you go you find people who are unable to walk, they linger about aimlessly as if they are not wananchi of Kenya.

Two; people who are insane, there medical services, the constitution should hope for that.

Land distribution should also be done evenly, not like where some few powers, when they get to powers, or they have a tones of land in the former European settlement schemes, which like fallow, whereas as if mwananchi here, has not even got 0.5 of an acre. The same big fish, has big office in Nairobi, has junks of land lying fallow in the settlement scheme, and our constitution does not allow, that junk of land, to be distributed to people who don't have the land. **(Interjection)**

Com. Salome Muigai: The last point.

Last point, human right; Kenya should be, should at least respect human rights, freedom of speech, freedom of assembly and e.t.c. Well thank you very much, I had more to contribute, but because of the limit of time, this is only my hand script, but I had humbly time to contribute my other views to C.J.P.C, Mvumo Parish, which I think have been submitted. Thank you very much.

Com. Salome Muigai: Eshikumo Roselyne, Patrick Nasitsi.

Patrick Nasitsi: Kwa majina ni Patrick Ngongo Nasitsi.

Langu ni kuhusu wezi. Unawezapata mtu ameshikwa, ameiba milioni kumi, kupelekwa kotini, bond wanasema, kwa mfano million mbili na msaidizi wake atoe million mbili, inabaki milioni sita. Hapo nitatumia kutatanisha ushaidi wa koti. Ni heru mtu akishikwa, kama mwizi, awekwe ndani kesi imalizike, ndio awachiliwe. Ama akiwachiliwa kwa bond, million kumi hizo, zishikiliwe.

Na upande wa pombe; sisi Waluhya hasa, tangu zamani, kufanya mambo yetu ya kimila, tunatumia busaa, sio chang'aa wengine wanazungumza kila wakati hapa. Busaa sio pembe yetu, hiyo ni ya Wanubii. Kwa hivyo, ningomba serikali ijayo, iruhusu busaa, maana mtu akifa, sherehe yake tunatumia busaa, na serikali itazidi kushika na kuumiza watu kwa ajili ya kukomesha busaa. Kwa hivyo, hiyo iwachiliwe.

Na upande wa recruitment kwa jeshi, nashangaa sana. Kwa Provinces zingine, nasikia watu wakipelekwa huko kufanya recruitment, wanachukuwa watu wa area hiyo. Na hapa kwetu, wakifikia hapa, tunasikia Njuguna amechuliwa hapa Butere, Ruto amechukuliwa hapa Butere, na ukifuatilia uwezi kupata Ruto amezaliwa hapa. Na vijana wetu wamezungushwa na kukimbia mbio, wanaachiliwa tu hivyo. Kwa hivyo, tungekubali serikali ijayo, ifuatilie sana, wakisema recruitment iwe hapa Butere, wawe watu wa Butere. Nafikiri ndio hayo tu nitasema.

Com. Salome Muigai: Asante sana. Roselyne amekuja? Isaiah Omulama.

Isaiah Omulama: My names are Isaiah Reverend Omulama.

About human rights; we are against the term as the president will be above the law. the only person or we only have God, who is above the law. and when the president has done any crime, he has to be taken to court, and at least meet the judgement.

Freedom of worship; we don't want such to go on, because we have a problem whereby, we have even devil worshipers, coming in between us, even in churches, trying to cheat people that, they are going maybe to take young boys and girls to school, and yet, you will find that boy or that girls, has been removed some blood with this devils, and he or she many die. So, freedom of worship, hiyo kitu hatutaki kwa vile unakuta ya kwamba, hayo yanaendelea katika makanisa. So we have no choices or strong laws, vile tulikuwa nayo. Ukifanya kitu kibaya, unapelekwa maybe kwa parish council, you are asked about the issues that you have done, and then maybe sent home. So, we find that, very many of us normally go to some other churches, and they continue with that evil thing that they have been doing in different churches. So, we should have discipline in churches.

Land division; I support my dear people have said that, this one has to take place even to ladies. Kwa maana tunakuta kwamba, unaweza kupatia kijana shamba lako, na pengine ule kijana, hana usaidizi wowote, unampatia, pengine anauza. Sasa tunakuta ya kwamba, hata wasichana, at the time of death, you get that girl, who can give maybe coffee, who can give a bull. Lakini mvulana anakaa tu hivyo. Kwa vile, sasa tunaona ya kwamba, hata msichana apatiwe uridhi, anaweza, unajua, akiwa mpole na mnyenyekevu, anaweza kugawia hata vijana.

The so we call, pombe haramu; as a Reverend, I have tried to look into this. This thing, tunaona ya kwamba, let us allow this people to drink this. Because even Sub Chiefs, Chiefs, are the people who are increasing this. Wanaenda pole pole, wanapatiwa elfu mbili, na pombe pengine kubuyu mzima, wanaendelwa kukunywa, halafu askari wakitembea, wanapita the other side. So, let us do like in Uganda, ile kitu iko tu kwa njia, and wacha wakunywe pombe, kutoka pengine saa sita, kuendelea. Na wakija kwao, walale. And if anybody is found maybe, drinking from morning without doing any work, let the government take that person to jail, for even seven years, and some seven strokes. Huyo mtu, yaani pombe iwe tu kialali, yaani nikitengeza pombe, isiwe ya kuuzwa. Tukunywe vile waafrica walikuwa wakikunywa kwa maboma. Ukienda kwa mwenzako, unakunywa tu pole pole, halafu mnaenda wapi, nyumbani. Hapana kutembea ukitaja jina yako, ati mimi ni nani, hapana. Mtu kama huyo, awekwe kwa jela, karibu miaka saba.

Na prisoners; I only thank the government, to have said that prisoners to see their wives is nice. But we want also, this prisoners with little crimes, at least to maintain our schools, yaani uchafu wote, hao watu wafanye, kulimia mahindi uko nje wafanye, kutengeza barabara, hao watu wafanye hiyo kazi, instead of them just congesting in prison, others maybe you find, they are dead. Lakini ile crime ambayo amefanya, pengine ameiba hindi peke yake. Tumweke kwa barabara, this rural road, walime wakitengeza, wabebe na ma wheelbarrows, hii nini, wakimwaga kwa barabara.

Na, majimboism; tunataka ya kwamba, tuwe na kitu kama in Western Province, we should have at least, some small president. That is, tuwe kama watu wa Kiangilikani, tuna ma bishops, lakini kutoka kwa ma bishops, kuna ule ambaye tunaita arch bishop.

Tuwe na president ambaye amefanyiwa elections, kutoka kwa hawa, ambao tumetoa katika Provinces. Halafu huyo mtu, atakuwa akiita hawa, ndipo wanaweza kudiscuss jambo. Sio, apitishie tu maneno kifuyake, lakini, awaite ndipo wamwambie, shida ambazo ziko kwa Provinces zao, na usaidizi at least tutapata. **(Interjection)**

Com. Salome Muigai: Last point, point ya mwisho.

Isaiah Omulama: Ningesema ya kwamba, yaani, tuna mila zetu. Mila zetu, tunatakiwa tufanye mila zetu. Ikiwa mtu anapasha watu wake tohara, afanye hivyo. Kwa maana sisi, kama Waluhya, mambo ya, this idea of circumcision, it shows somebody who is maybe a grown up, who is ready to marry, and it should be done in various places. Kama Wajaluo, wawe, wakitooa meno watoe, na sisi tufanye vile tunavyo.

Com. Salome Muigai: Nina swali moja kwako.

(Inaudible) Kama jambo la

kutoza tohara, na ni kubwa katika kwa Kiluhya. Lakini wakati huu tena sasa tuna ugonjwa huu wa ukimwi. Je, tutahitaji kuangalia hayo mambo mawili pamoja, na tufikirie vile tunaweza kuyajumuisha vipi ili yote ifanyike, lakini sio ya watoto wetu wa kike.

Isaiah Omulama: Tunaweza kurekebisha, kwa vile tulikuwa na wale ambao wanafanya hiyo kazi, tunaita kwa Kiluhya Kimrere. Sasa tukitoa mambo ya kutumia ile kisu yetu, ile ya hapo awali itakuwa vizuri. kwa maana huwa wanatumia

(Inaudible) na nimekuta ya kwamba, hiyo sasa ina

(Inaudible). Na daktari unajua, tena ni vigumu,

unakuta mwanamke, tena anafanya hiyo kazi kwa mwanaume, na it is a problem to we men. Mwanamke anatahiri kijana, it is wrong.

Com. Salome Muigai: Haya ni maoni, ni wakati wa kufikira mila zetu na maendeleo yetu pamoja, na kufikiria vipi tutakuwa nayo pamoja. Habil Nabanga.

Habil Mavango: Mimi ni Habil Mavango Wamboe. **(Interjection)**

Com. Salome Muigai: Mavango?

Habil Mavango: Yes.

Com. Salome Muigai: Endelea.

Habil Mavango: Maoni yangu, niko kwa ni kwa ugonjwa wa ukimwi. Ugonjwa wa ukimwi inashika watu. Nayo serikali, inaona mimi niko na ugonjwa, na inaniwacha tu mimi naendelea, kupanbasa hiyo ugonjwa. Nimefikiria sheria ikuweko, nikipatikana niko na hiyo ugonjwa, niwekwe mahali peke yangu.

Neno la pili, ni mambo ya walimu kwa shule, na watoto. Mwalimu anapatia mtoto mimba, na yeye huyo ni mtoto wake. Nayo serikali, iwezi kuingilia hiyo neno. Lazima hiyo mwalimu, atafanya transfer kuenda mahali, na sasa anaenda na huyo mtoto. Miaka kidogo, anawacha huyo mtoto. Nimeomba, sheria ikiwa inaweza kutupatia sheria fulani, ya mwalimu akiwa amefanya hivyo, iwekwe. Ni hayo tu mawili.

Com. Salome Muigai: Ungetaka afanywe nini huyo mwalimu.

Habil Mavango: Huyo mwalimu akiwa amechukua mtoto wa shule, ni heri afutwe hiyo kazi.

Com. Salome Muigai: Na akitunza mtoto anafanywa naye nini mzee.

Habil Mavango: Alipe mahari, pesa ya ule baba wa huyo mtoto.

(Inaudible).

Com. Salome Muigai: Asante sana mzee Habil. Jackson Omwaka, Patrick Omanyo, karibu.

Patrick Omanyo: Kwa majina ni Patrick Omanyo. Ningependa kuchangia Tume ya Marekebisho ya Katiba.

Nikianza na upande wa kazi; unapata kuna watu, ambao wameandikwa kazi na wanapata mshahara mwingi. Hapa, ningependekeza, wameandikwa na wanapata mshahara mwingi, mshahara upunguzwe, na tena, mtu mmoja akuwe na kazi moja. Kwa sababu kuna mtu mmoja ambaye ako na kazi hata zaidi ya saba, na zote anapata mshahara.

Wabunge, wakichaguliwa kuenda Bungeni, wakifika huko na wafanye makosa, sisi wananchi ambao tuliwachagua, tuna haki ya kuwaita warudi na tufanye uchaguzi mpya.

Kuna kile kitu tunaita hazina ya raisi, nafikiria hii hazina ingeondolewa. Na, badala ya kuwa hazina ya raisi iitwe, hazina ya watoto mayatima.

Raisi akistaafu, asibaki kama mwenyekiti wa chama. Hii ni kwa sababu, akibaki kama mwenyekiti, atakuwa ako na mamlaka, hata kushinda raisi.

Wabunge wateule; nafikiria jambo la Wabunge wateule lingeondolewa. Kwa sababu ikiwa watu wako wamekukataa na kuchagua Mbunge mwingine, wewe unapelekwa huko kufanya kazi gani?

Ndoa; ningeomba ndoa iunganishwe na kanisa, wala sio serikali. Kwa sababu unapata, kuna mahali ambapo unapata mzee ameo, anafanyishwa ndoa na kanisa, na tena baadaye unapata, aliowa bibi mahali pengine, na akaenda katika serikali, akafanya huko ndoa tena.

Kuna mahali ambapo mtu unapata ako na kazi, na unapata, anawacha ile kazi kuenda kutafuta kazi ingine. Ni heri, mtu ashikilie ile kazi yake ambayo alipewa, ambaye alijivunia, pengine atapata maarifa kwa hiyo kazi. Na wale wengine ambao hawana kazi, wapigane kiti cha ile kazi ambayo imetoka.

Kuchapwa kwa walifu; kivyangu ningeon, kuna waalifu ambao ushikwa na kuanza kuchapiwa tu hapo. Ni heri sheria ingekuwa, muaalifu akishikwa, aende mpaka kotini, koti ikate ukumu kwamba, anafaa kuchapwa, ndio achapwe. Asante.

Com. Salome Muigai: Asante sana, jiandikishe tafadhali. Wycliff Omanyu, Emily Mwale.

Emily Mwale: Kwa majina ni Emily Mwale. Maoni yangu, ni kuuliza hivi;

Ma Councillors, Wabunge, President; kwa nini hawapewi miaka ya kufanya retire.

Com. Salome Muigai: Ungependekeza jambo gani, ungetaka kuona nini?

Emily Mwale: Wawe na lengo ya miaka yao, wafanye retire, pengine waende.

Neno la pili; nafikiria kwa maoni yangu, naona, ma Chief, na Assistant Chief, wakipata hiyo kazi, waende kwa country ingine, na wengine wakuje kwa country yao. Waje kufanya kazi kwa country yao. Wakiendelea kazi kwa country yao, wanakuja na maneno ingine.

Nakuja upande wa mama na baba, kwa boma. Upande wangu, naangalia tu kwa ma boma, awe naona hata kwangu. Unaona mwanaume ako na ng'ombe na ana kazi kwa boma, lakini asubuhi anaoga tu anatoka. Na saa ya kurudi, anataka kukula, na wewe unaendelea na kazi yako, ufanye kazi uende kwa shamba, uchungu ng'ombe, utafute mboga, na akirudi, anauliza kukula.

(Interjection)

Com. Salome Muigai: Ungetaka tufanye nini mama?

Emily Mwale: Lazima huyo mzee naye aende kwa shamba, akusaidie kazi ndio atoke.

Maoni ya tatu,

Com. Salome Muigai: Tafadhali mkiwa mnasimamia akina baba watoe maoni yao, nitasimamia akina mama watoe maoni yao.

Emily Mwale: Akina baba, anakuletea ama anakupa punishment asio na maana.

Com. Salome Muigai: Anakupa nini?

Emily Mwale: Punishment. Kwa maana ukitoka kwenu, unakuja kuolewa kwa boma ya mtu, sio wewe ni mfanyi kazi. Na sasa sisi tukiolewa, tunakuja tu kufanya kazi kwa maboma ya watu, sio ati sisi ni wanawake. Hapo mnaweza kusaidia hao balaa.

Com. Salome Muigai: Haya tueleze vile ungetaka mama, ungetaka tufanye nini, ungetaka sheria ikusaidie na nini?

Emily Mwale: Sheria itusaidie tukuwe tu wanawake wa kuolewa kwa boma ya watu, sio ati tukuwe wafanyikazi.

Zamani za kale, siku ya mimi nilikuwa kwa shule. siku ya mimi nilikuwa kwa shule, hiyo miaka kidogo, ama miaka moja mbili, niliona serikali inakusaidia, ingwen, ink na kalamu. (**Interjection**)

Ingwen ni nini, ingwen, na biro, na vitabu hata vya kusoma. Siku hizi mimi ni maskini, na tena nilitoka kwa jamii masikini, nataka mtoto wangu asome. Na siwezi kununua hivyo vitu vyote, nipatie mtoto, sasa nifanye nini? (**Interjection**)

Com. Salome Muigai: Ungetaka nini?

Emily Mwale: Nataka serikali kama inakubali, itusaidie kwa hiyo maneno. (**Interjection**)

Com. Salome Muigai: Mama leo una siku yako ya kueleza vile ungetaka.

Emily Mwale: Nataka itusaidie, kwa maana hata mimi nilitoka tu kwa jamii masikini, hata hii nguo navaa, ni ngugu yangu ananisaidia kununua. Hata mtoto wangu, yeye anakuja kwa shule, ndugu yangu ananisaidia na dada yangu, sasa hawawezi kukubali, kusaidia mimi, wasaidie watoto, na tena kupeleka kwa shule. Wanaweza kweli? Sasa nitakuwa tu jamii masikini mpaka siku yangu ya kifo? Mnisaidie hapo, ndio ile neno nataka mnisaidie nayo, watu wa serikali kama mnataka kutusaidia, mtusaidie na hiyo.

Com. Salome Muigai: Asante sana, kwa maoni yako. Alfred Omukanda.

Alfred Omukanda: Jina ni Alfred Omukanda, kutoka West Marama, Butenya sub location. Ningependa kuleta maoni yangu kidogo, hapa.

Ya kwanza; president achaguliwe na watu.

Ya pili; tuwe na busaa kila sub location. (**Interjection**)

Com. Salome Muigai: Tuwe na nini.

Alfred Omukanda: Busaa

Com. Salome Muigai: Busaa?

Alfred Omukanda: Eeh, local beer. Hiyo itamarisha hao ma Assistant Chief, wasiwe na hasira na watu, ikiwa serikali itapeana hiyo.

Assistant Chief, achaguliwe na watu.

Mwanamke, asiwe na mamlaka kushinda mwanaume.

Watoto wasome kutoka darasa la kwanza, mpaka darasa ya nane, bure. Serikali igharamie hiyo.

Msaada; tuna barabara mbaya, katika mahali, County Council wanatoka, kama Butere Country Council, ama mahali popote. Hiyo barabara ningependa, ikiwa kama sheria ikitoka, Country Council itengeneze hiyo ma barabara. Ni hayo tu machache.

Com. Salome Muigai: Thank you Alfred na muda wako umeutumia vizuri. Silas Akhusama.

Silas Akhusama: Kwa majina naitwa Silas Akhusama, from Marama North, Naya sub location.

Mimi ningependekeza, president anayechaguliwa, awe ndio chairman wa chama ambayo kimemchaguwa. Tusiwe na chairman kando, kwa sababu akitaka kuitisha mikutano itakuwa ngumu.

Ya pili; askari anapotoka stesheni, au askari awe AP, awe Police, ati anaenda kushika mtu yeyote ambaye amerepotiwa amefanya makosa. Lazima awe kwa uniform. Tena, katika hiyo uniform, awe na nambari yake ya kazi. Kwa mfano, tuna administration police, hawana number ya kazi, na sisi hatuwajui, kwa maana ni mtu amekuja, ameletwa kutoka mbali, na hiyo ndio safari yake ya kwanza kuona yeye. Na akikumiza, hiyo number unaweza shika na utoe malamiko yako, malalamishi yako, kwa ule ambaye, mahali unatakiwa upeleke.

Na, wakienda kufanya kazi wale police, lazima wawe na mtawala wa hapo. Kwa sababu, yeye ndio anakujua. Wasitoke huko na kuingia kwa boma ya mtu, kama mnaingia kwa msituni. Wawe na mtawala wa area hiyo, ndio utamtambua kwanza.

Inginge; civil cases, zifanywe na watawala wa huko, kama Chiefs, na wale ambao wako chini yake. Wakishindwa, ndio wakupeleke mbele.

Criminal cases; kwa maana criminal case ndio inahitaji sana askari kwa sababu ana silaha. Ndio sababu ule Assistant Chief, au ni Chief, anaweza kuenda kuitwa wale maaskari, wakiwa hapo armed. Labda huyo mtu amevunja nyumba, au ameingilia mtu amemuumiza, anahitaji tena force ya aina hiyo. Ndio askari wanaweza ingia hapo, na kushika huyo mtu, na apelekwe huko

mbele straight, wasikalishe kesi hapo ya criminal case, kwa maana hiyo iko very serious.

Kwa upande wa mashamba, ikiwa mwanamke atakuwa na haki ya kuridhi shamba, basi tena awe na haki ya kuowa mwanaume, na kumleta kwa hiyo shamba. Na kama awezi kuowa mwanaume, basi mwanaume ndio anafaa awe mridhi wa hiyo shamba. Ni hiyo ninao, wengine wanataka kuongea, ninawachia hapo.

Com. Salome Muigai: Asante sana. Ambaye Nyenje, Nyenje ama Nyenja, James Okama.

James Okama: Well I am James Wetaba Amos Okama, kutoka Marama West, Bukunya sub location, an elder for Abachenyaba clan. **(Interjection)**

Com. Salome Muigai: Inaudible

James Okama: Well, katika Constitution of Kenya Review Commission, mimi nina haya ya kusema;

Kwanza, katika Kenya, hatuna, tulikuwa hatuna preamble. Na mimi napendekeza ya kwamba, it is necessary to have a preamble in our constitution.

Two; we Kenyans by origin, should feel protected in all our endeavours mechanism, security, employment.

Directive principles; Kenyans should have important values to reflect in the constitution, such as, traditions, customs and complexion, e.t.c.

When we come to constitution supremacy, where we have a parliament; parliament should have the supreme powers of amending all parts of the constitution.

I come to citizenship; automatic Christian, citizen of Kenyans should be this or those or in Kenya or outside Kenya, by both parents who are Kenyans. Born by a Kenyan father.

Three, outside women getting married men, Kenyans citizenship should also be acquired by registration, for not less than 15 years e.g. outsiders marrying Kenyan women, because they shall be bound to visit and taken care of the women,

(Inaudible)

I come to political parties; number of political parties should only be limited to three parties.

Where we come to political parties, should be financed through donors. Public fund should be challenged to public development and not on political issues.

Structure and system of the government; we should adapt a federal system of government, this is majimbo, in which, executive and legislative authority is simply between the central government.

Regional unit to address the activities carried out in those such a region.

Jambo ya mwisho, nakuja kwa elections; election system, election, watu wana haki ya kumchagua president. Wawe na uhuru wa kuchagua president, na wawe na uhuru wa kuchagua M.P. Na ikiwa an M.P amefanya makosa, anaporudi katika area ambayo alichaguliwa, wale walimchagua wawe na votes of no confidence immediately, wamwondoe na wamchaguwe mwingine, kwa kipindi hiyo hiyo.

Na hii yote, hata yale mimi bado sema, nimeandika chini, na itakuja kuangaliwe huko, ninapopeana karatasi.

Com. Salome Muigai: Asante, Elphas Oweri.

Elphas Oweri: Mimi ni Elphas Oweri.

Maoni yangu, ni ile ya baba akikuwacha shamba. Baba akiwacha shamba, inatakiwa, kama hapana wacha mtoto wake wa kiume, inatakiwa ule ndugu yake ambaye anamfuata yeye, afanye uridhi kwa shamba hiyo, halafu wale watoto ambao alikuwa amewacha wadogo, wachukuwe hiyo shamba.

Na vile walisema ati serikali sasa vile, ilichukuwa wakati wakufunga shamba, walisema watakaa kwa shamba miaka mia moja. Miaka mia moja hiyo, itakuwa kama hao watoto kidogo kidogo watazaana na halafu anawacha, wanaendelea kwa shamba hiyo. Mimi naona tu kama, ukiweka ile nini, ukiweka msichana, msichana wako kwa shamba sio mzuri. Kwa maana wale ambao watabakia hapo wa ndugu yako, watakataa. Watakatakata hiyo, watakatakata, wataleta fujo, na watakatakata huyo msichana unawacha kwa uridhi kwa shamba lako. Ni heri tu ndugu yako aridhi hiyo shamba, na atatangulia wale wengine, watakaa watoto wale unawacha kama bado (Inaudible).

Kwa kutahirisha; kwa kutahirisha, inaleta ugonjwa, ugonjwa ni nyingi. Kwa maana wanakambatwa wanaenda hospitali, wanakatwa hapa, wanakatwa na daktari na makasi ni moja. Ni heri warudi vile walikuwa wanatahirishwa zamani, ingekuwa vizuri, watazui magonjwa. Kwa maana wanaambukizana. (**Interjection**)

Com. Salome Muigai: Unaweza twelezea vile zamani ilikuwa?

Elphas Oweri: Walikuwa wanatahirisha tu na watu wawili, na kisu moja. Na akiwa kilema, kama alizaliwa mapacha, yaani twins, anafanya nini? Ako na kisu yake, kwa maanu ule mtu anatembea na kisu, kila aina ya kisu. Na kwa hivyo, hapo kutahirishwa inaweza kuwa namna hiyo.

Na, mwanamke akipewa mamlaka; mwanamke akipata kazi, mimi nafanya kazi Nairobi, na mwanamke ako Mombasa, akiwa na kazi yake, yeye anapata bwana uko, na sasa mim nabakia bure, hiyo ni mbaya, ni makosa. Sasa, vile wanawake walipat kazi, wanadharau bwana yake ule ambaye alifanya naye ndoa.

Sasa ana kwenda kupata ya ile ingine. Sasa unabakia bure sasa, sasa utaoa namna gani, hiyo watoto anawachia wewe, saa ingine anakuja kunyang'anya wewe watoto wote, anakwenda nao. Unabakia kama ukiowa bibi, na wewe ndio ulitoa mali. Kwa hivyo si mzuri, mimi naona kama mbaya.

Wakati tulikuwa tunasoma hapa, 1952, hapa, hii ndio ilitoa hii shule, hii mawe hii, mabadiliko iko sasa. Sasa wasichana, watoto wa siku hizi, wakienda kunywa pombe, yeye anakuja kuenda kuuza shamba tu. (Inaudible) Sasa vile unaweza kuenda huko kutoa hiyo shamba ni ngumu. Na wewe sasa ni mzee.

Com. Salome Muigai: Ungetaka tufanye nini mzee?

Elphas Oweri: Hiyo sasa ilikuwa inatakiwa, wasipewe ruhusa kuuza shamba na mtoto, wasikubali kuuzia tu huko bila kujua. Unaona tu mtu mwingine yuko kwa shamba.

Tena kuuza mashamba, hata wanawake wale ambao mnasema, wanataka wapewe mamlaka, wanauza shamba kwa kujenjekea. Tena mzee amekwisha kufa, watotot wake wanataabika, hapana sema, hapana soma. Na Sub Chief, au Chief, au D.O, awezi kujua watoto wanataabishwa. Watoto wako bure tu, wanawachwa bila kusoma. Huyu mama anaenda kwa bwana mwingine. Anauzia mdosi mkubwa, mtu mkubwa, na kwenda nayo, anaama na shamba. Anauza halafu anapeleka yeye kwake, na watoto wanabakia kwa taabu.

Hiyo ndio maoni yangu, kama wanaweza kurekebisha, wanaweza kusaidia.

Com. Salome Muigai: Mzee mimi nina swali moja kwako. Nimesikia akina mama wanauza mashamba, watoto wanauza mashamba, akina mama wakipata kazi wanawacha bwana na kuenda kuolewa na bwana mwingine, si wewe mzee siku moja umeona bwana mwenye ameenda kwa kazi na kuowa bibi mwingine, ama umeona baba mwenye ameza shamba na kuwacha watu wake kwa shida.

Elphas Oweri: Ni wengi.

Com. Salome Muigai: Okay asante, jiandikishe mzee asante, Hannington Chite, Edward Outa.

Edward Outa: Majina ni Edward Outa Omanyoo. Yangu ni machache kwa hii.

Com. Salome Muigai: Utangoja tafadhali, naona nyinyi mmalize kwanza, mmaliza kunena, tafadhali tumsikize huyu.

Edward Outa: Yangu kwa new Commission Review ya Kenya ni machache sana.

La kwanza ni uridhi ya shamba. Ningependelea, kama mimi ninakufa, nawacha shamba langu, tusiwe na mambo ingine ati mtu anaenda kotini kubeba kitabu, kuapa mbele ya koti, ndio achukuwe shamba. Kuna Chief, kuna Assistant Chief, yule ananijua mimi. Yeye ndio anatakikana atoe barua. Kama ni watu wangu kuenda kwa lands, waende kwa lands, shamba ibadilishwe kwa ule nimewacha. Shauri hata tumeshaona ni wengi wanabeba vitabu, kuwapa ni hivi, lakini wanabeba kwa njia ya uwongo.

Ingingine, ni mambo ya skuli, walimu na wanafunzi. Kuna wazazi wengine wale hawajiwezi, hawana pesa, mtoto anafanya mtihani, anapita vizuri, anaitwa Alliance. Ametoka Busia, anaenda Alliance, Alliance ni Kikuyu ni mbali. Mtoto ameshaenda Alliance, na mzee ni ule mtu wakutafuta pesa kwa kiasi ndio apate, ndio alipe school fees ya mtoto. Mtoto anafukuzwa kutoka Alliance ama kutoka Kilifi, aje Busia kupewa school fees na mzazi. Hiyo kitu ya kufukuza watoto kwa shule kuenda kutafuta pesa kutoka kwa mzazi, ninaonelea ingetolewa. Kama mzazi ajatoa pesa, skuli iandike barua ienda kwa huyo mzazi, ikimuliza pesa, kama inawezekana, apate pesa, alipe. Shauri hakuna faida, mtoto amebaki na shilingi elfu moja, wanamfukuza kwa shule kutoka Kilifi, kuja Busia, ni karibu shilingi elfu mbili kuja na kurudi. Hiyo ni gharama ingine kwa mzazi.

Com. Salome Muigai: Endelea mzee.

Edward Outa: Lingingine, Assistant Chief na Chief; tangu zamani, walichaguliwa na watu, na wanachaguliwa na watu shauri wanatoka kwa hiyo kabila, hao ndio wanajua maneno ya hiyo kabila. Mimi ngingeonelea, Chief na Assistant Chief, tangu zamani alikuwa anafanya kazi, kwa ile location, au ile division, ile yeye yuko. Shauri kutoa hapa Chief, kupeleka yeye huko Kikuyu, ajui manenoya Wakikuyu, afanye kazi pahali alichaguliwa. Hiyo nimewacha

Maneno ingine ni , askari wa polisi; askari wa polisi, wana kitu kimoja, ile wanaona wafanye. Na hiyo kitu ni pombe peke yake. Ukiita police mtu amekufa, yuko hapo kwa nji, atamaliza three hours hapo, kama police ajapita. Lakini ukimwita umwambie, kuna watu fulani wamekunywa pombe mahali fulani, itawachukuwa half an hour kufika hapo. Tunataka kitu kama hiyo, serikali ikiweza, itusaidie.

La mwisho, ni mambo ya ushahidi kotini; mimi nimebaka msichana, namshika namnajisi. Nikinajisi mtu, sidhani kama kunako

mtu karibu anaona, shauri kuna jinsi pengine, upate mtu kwa kichaka mahali, ndio umnajisi. Ili neno ati mtu anaulizwa kotini nimekunajisi, unaulizwa, leta mashahidi. Hiyo kitu iondolewe, wewe sio wazimu, utaenda kushtaki mtu anakunajisi, kama hajakunajisi.

Lingine, ninekutana na mtu, tumekutana wawili, tumechokozama, mtu ananikata na panga. Kuna alama ile inaonyesha nimekatwa na panga, ninaenda kotini, inakuwa, leta mashahidi. Tulikutana wawili, mashaidi alikuwa wapi? Mashaidi wangu nataka, ni ile alama niko nayo kwa mwili, na ile daktari ameniona wakati nimeumia. Yangu nimefika hapo madam.

Com. Salome Muigai: Asante sana, tafadhali jiandikishe, Jackson Ondati.

Jackson Ondati: Jackson Ondati, the current Chief, Marama, Western.

The previous speakers, are my subjects, and at times, they have been touching on me. **(Interjection)**

Com. Salome Muigai: Bwana Chief, leo tunazungumzia habari ya kila mtu anvyoona, sio kwa ajili yako, au kwa ajili. Umesikia wakisema wanawake wasipate madaraka?

Jackson Ondati: Ndio.

Com. Salome Muigai: Lakini bado nimewapa nafasi na nikawa protect. Kwa hivyo, excuse me, kwa hivyo leo ni siku ya mazungumzo, mtu akisikia tu asikie yeye anahusishwa.

Sasa, nilikuwa nataka kusema hivi **(Interjection)**

Com. Salome Muigai: Wamekuwa na ma Chief kutokea wazee walipokuwa watoto wadogo, kwa hivyo wameona Chief wengi, sio wewe peke yako. Kwa hivyo, tafadhali usichukulie hili kuwa wanakulenga wewe. Hata mimi wanaposema hawataki wanawake wapate madaka, hawanilengi mimi, wanazungumzia kwa jumla ya mambo.

Jackson Ondati: Nilikuwa nataka kusema hivi, sikusikia vibaya, lakini nilikuwa nataka kusema **(Interjection)**

Com. Salome Muigai: Lakini wewe toa maoni yako, kulingana na hako yako.

Jackson Ondati: Maoni yangu kuhusiana na kazi yangu, ambayo ninafanya saa hii, iko hivi;

Ninaanzia kwa maendeleo, kwa maana kazi yangu inahusiana na security na maendeleo. Sasa katika maendeleo, lazima tuwe na

foundation mzuri. Na foundation mzuri ni elimu. Ninapendekeza hivi; hizi early childhood development, ni kitu ambacho ninapendekeza iwe ya lazima na hizo shule zijengwe na local government. Na hata hao walimu walipwe na hao.

Com. Salome Muigai: Endelea.

Jackson Ondati: Domestic violence, ugomvi kati ya bibi, na bwana. Huo usuluhishwe na wazee wa kijiji.

Tuko na civic education, ambayo imeletwa tu kilingana na maneno ambayo tuko nayo kwa saa hii. Mimi ningependekeza, iendelee, iwe ikiendelea throughout. Kwa maana mimi naona bado tuko na ignorance, katika country hii. Civic education iendelee mpaka chini kabisa, ndipo tuweze kumaliza hii maneno ya domestic violence.

Maneno ya mashamba, land boundary dispute; tuwe na sub locational elders committee, ya ku deal na hizo problems.

Nikiwa hapo kwa maneno ya mashamba, yule mtu ambaye ako na chini ya acre mbili, na ako na zaidi ya miaka kumi na nane, serikali iangalie ipeane mashamba kwa hao watu. Shamba iwe na familia.

Wale ambao wamepeanwa kulinda sheria, kuona sheria inatekelezwa, wawe, wapeane uwezo wa kutengeneza hiyo sheria, bila kuingiliwa na mtu yeyote. Wale, narudia, wale ambao wamepeanwa jukumu la kulinda sheria, kitu kama security, usalama, wawe, wapeanwa uwezo, wa kufanya hiyo kazi na wasiingiliwe na mtu yeyote.

Tuna petty cases, ambapo mtu ametukama mwingine, na tuna ushahidi. Hiyo kesi imefika kotini, sioni ni kwa nini inaahirishwa mwaka mzima. Hiyo kesi ikifika kotini, ushaidi uko, ichukuwe hata iishe siku hiyo. Kama ushaidi hakuna, huyo mtu awe released, kama ushaidi uko, huyo mtu afungwe siku hiyo.

